



**KIBABII UNIVERSITY COLLEGE  
(KIBUCO)**

**MAIN CAMPUS**

**UNIVERSITY REGULAR EXAMINATIONS**

**2014 /2015 ACADEMIC YEAR**

**3<sup>RD</sup> YEAR 1<sup>ST</sup> SEMESTER EXAMINATION**

**MAIN EXAMINATION**

**FOR THE DEGREE OF BACHELOR EDUCATION (ART)**

**2 Hours**

**COURSE CODE: KIS 315**

**COURSE TITLE: LITERARY DEVICES AND CRITICISM**

**DATE: 15<sup>th</sup> January 2015**

**TIME: 8.00-10.00 a.m**

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES:**

- Jibu swali la kwanza (**LAZIMA**) na mengine mawili

1. (a) Fafanua dhana zifuatazo: (alama 10)
  - i) Nadharia
  - ii) Fani
  - iii) Falsafa
  - iv) Halimahasa
- (b) Jadili namna S. A Mohamed alivyotumia uhuru wake katika kuiandika riwaya ya *Asali Chungu* (alama 10)
- (c) Fafanua dhima ya uhakiki katika kazi za fasihi (alama 10)
2. Pambanua umuhimu wa mandhari katika ujenzi wa maudhui kwa kutoa mifano maridhawa kutoka katika kazi zozote za sanaa (alama 20)
3. Kwa kurejelea mifano kutoka katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* Ken Walibora, fafanua kaida za msuko (alama 20)
4. Changanua kwa ufupi mikabala yoyoye mitano inayotumiwa kuhakiki kazi za fasihi (alama 20)
5. Hakiki shairi lifuatalo kwa kuzingatia fani na maudhui: (alama 20)

## VINYAGO

Waangalieni

Wale wanaotuongoza

Wanavyochechemea

Wanavyopepesuka

Mara huku mara kule

Mara hapa mara pale

Kila mahali ulimwenguni

Wale wanaotuongoza

Pingu mikononi

Pingu miguuni

Pingu maningani

Na bado wanatufanya vinyago vya sakarani

Wametucheza watumwa

Nyuso chafu kama kilabu

Tumecheka tukilia bila sababu

Mikono tukiipepepa kama madubu

Mpaka.....

Tumekuwa mabingwa wa michezo wa mtumwa

Katika hili jukwaa la dunia

Tumeshindana katika huu mchezo waliotufunza

Tukicheza miili yetu, tukiitambaza kama mafunza

Tukipanua makanwa na midomo

tukitingisa matako na viuno

tukitoa mashuzi na misono  
huku haya zote tumezibana  
Haya basi, tupigeni mayowe  
tupigeni makofi  
    ili wakuu wacheke  
    ili wakuu wafurahike  
    Haya!  
    Haya!  
    Haya!  
Hiyo ndiyo kazi yetu,  
Kwani tu vipofu  
Kuliko hao vipofu!